KARADHA TANZANIA

Muhtasari wa shughuli za Karadha –Julai, 2005

Mradi wa Karadha Tanzania (SECO IFC LEASING PROGRAM TANZANIA)

©Haki zote zimehifadhiwa.

Hakuna ruhusa ya kunakili sehemu yoyote bila idhini ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC). Taarifa zilizoko humu hazijahakikiwa pamoja na kuwa zimepatikana kwenye vyanzo vinavyoaminika, Shirika la fedha la kimataifa (IFC) halitoi hakikisho la usahihi wake.

Taarifa hii pia haimaanishi kuwa msomaji anakaribishwa kuwekeza kwenye karadha, kwa kuwa IFC haijasajiliwa chini ya Sheria ya washauri wa uwekezaji ya Marekani ya mwaka 1940. Majina na sehemu mbalimbali zilizotajwa humu zimetumika kusaidia kutoa ufafanuzi tu, na sio msimamo wa IFC au Benki ya Dunia au taasisi nyingineyo inayohusika na Benki ya Dunia.

Tahariri

IFC ina malengo ya muda mrefu ya ukuzaji wa karadha kwenye nchi zinazoendelea. Kati ya Aprili na Julai 2005, IFC ilifanya utafiti hapa Tanzania kubainisha mambo yanayozuia kuendelea kwa karadha. Karadha ni aina mpya ya kufanikisha kupatikana mali kwa ajili ya shughuli za biashara. Karadha imekuwepo kwa muda mfupi na imewezesha wajasiliamali kadhaa kupata mali zenye thamani ya dola za Kimarekani (US$) milioni 35.2 ambayo ni chini ya asilimia mbili (2) ya pato la taifa. Karadha kama njia mbadala ya kupata mali za uwekezaji, inawafaa zaidi wafanyabiashara ndogo na za kati ambazo huchangia asilimia 90 ya pato la taifa na wana mahitaji makubwa ya mitaji.

Utafiti ulioendeshwa ulipata maoni ya wadau mbalimbali kwenye sekta ya fedha, serikali, makampuni madogo na makampuni ya kati (biashara ndogo na za kati), wataalamu na washiriki wa sasa wa karadha. Utafiti pia uliangalia mfumo wa kisheria unavyoathiri maendeleo ya karadha.

Utafiti huu ulibainisha maeneo matatu yanayosababisha karadha isiendelee na kutoa mapendekezo ya marekebisho yanayotakiwa ili kuweka mazingira mazuri ya karadha hapa Tanzania.

Vizuizi hivyo ni pamoja na:

(a) Kutokuwepo sheria inayosimamia karadha, ikiwa ni pamoja na baadhi ya sheria kutumika vibaya kumlinda mkopaji wakati mkopeshaji akitaka kupokonya mali iliyo kwenye karadha pale ambapo mkopaji ameshindwa kulipia karadha.
(b) Kuwepo kwa vivutio vichache vya kodi kwa wakopeshaji na kodi ya ongezeko la thamani kwenye malipo ya karadha na hivyo kufanya karadha kuwa njia ghali zaidi ya kupata mali.

(c) Kutotambulika kwa karadha hapa Tanzania.

IFC inatoa mapendekezo yafuatayo:

(a) Kupitishwa Sheria ya karadha;

(b) Kuwepo nafuu ya kodi kwenye karadha kwa wakopeshaji ili kuvutia washiriki kama vile mabenki na asasi nyinginezo;

(c) Kurekebisha Sheria ya ongezeko la thamani kwa ajili ya kuwezesha karadha ya fedha kutumiwa na wadau kama njia mbadala ya kujipatia mitaji ya kuendeshea shughuli za kibiashara

(d) Kuendelea kutoa mafunzo na elimu kwa umma kuhusu karadha hapa Tanzania.

IFC itatoa mapendekezo kwa Serikali jinsi ya kuendeleza karadha hapa Tanzania.

SECO IFC LEASING PROGRAM TANZANIA

IFC inatekeleza mradi wa kuendeleza karadha hapa Tanzania (SECO – IFC Leasing Program - Tanzania) ili kukuza na kuendeleza karadha. Mradi huu unatekelezwa kwa msaada wa kitaalamu unaotumia uzoefu wa IFC kutambua matatizo yanayoikabili sekta binafsi hapa Afrika na ushauri ambao imetoa kwa serikali mbalimbali na taasisi binafsi kuhusu namna yakukabiliana na changamoto hizi.

Lengo la SECO IFC Leasing Program Tanzania ni kuongeza ufanisi wa njia za kupata mitaji kupitia karadha, hasa kwa wafanyabiashara ndogo na za kati ; na hivyo kuongeza uwezo wa makampuni hayo kutumia karadha kama njia mojawapo ya kupata mitaji.

SECO IFC Leasing Program Tanzania imefadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia shirika lake la Maendeleo (SECO) na IFC.

Wafanyabiashara ndogo na za kati wameshindwa kupata mitaji kutokana na gharama kubwa zinazotakiwa na njia nyinginezo za kupata mitaji kama vile mikopo ya benki, kutokuwepo njia mbadala ya kupata mtaji na kuwepo kwa wigo mdogo wa soko la mitaji hapa Tanzania.

Karadha ni njia mojawapo ya ziada ya kupata mitaji na kuwezesha makampuni kutumia njia zote za kupata mtaji wa muda mrefu.

Karadha ya fedha ni njia ya muda wa kati ya kupata mitaji kwa ajili ya uwekezaji. Karadha huwezesha kupata mali hizi moja kwa moja bila kuhitaji fedha za kulipia mali hizo ambazo ni nyingi na kuendelea kuzilipia kadri zinavyoendelea kutumika kwenye biashara.

Wakopeshaji, ambao wanaweza kuwa mabenki, makampuni ya bima, watengenezaji wa mali, wauzaji au taasisi za fedha; hununua mali husika na kuziweka kwenye karadha ambapo hupokea malipo yanayohusisha matumizi ya mali hiyo. Mwisho wa karadha, umiliki unaweza kuhamishiwa kwa mkopaji, mali ikauzwa au kama imeshatumika huachiwa mdau mwingine.

Karadha hutegemea kutoa faida kwa mkopeshaji kutokana na malipo ya karadha ambayo ni ushuru wa matumizi kuliko umiliki wake na kuangalia kwa karibu zaidi uwezo wa mkopaji kulipia ada hii.

Karadha ina nafuu kwa biashara mpya ambazo hazina mtaji na hazina historia ya utendaji ambayo ingeziwezesha kupata mkopo kutoka kwenye taasisi za fedha au zina mali ya kuweka kama rehani.

Karadha imekuwa ni chanzo kimojawapo kwa wafanyabiashara ndogo na za kati kupata mitaji. Karadha huchangia kuongeza idadi ya mali walizonazo wafanya biashara ndogo na za kati, hususani makampuni binafsi au mapya ambayo yana nafasi ya kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi.

Lengo kuu la mradi ni pamoja na:

(1) Kuwezesha kuwepo sheria za kusimamia karadha – sheria zilizopo na ile ya karadha inayotegemewa kupitishwa, zitaangaliwa ili kubainisha mahali ambapo zinapingana ;

(2) Kuongeza uwezo wa wataalamu kupitia mafunzo kwa wabunge, wataalamu wa fedha, wakopeshaji, taasisi za fedha na wakopaji ;

(3) Kuendeleza biashara kwa kuunganisha wadau wote ambao ni wafanya biashara ndogo na za kati, watengenezaji wa mali zitakazokuwa kwenye karadha, na asasi za fedha ;

(4) Elimu kwa umma – kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu karadha kwa kupitia majarida, semina, vyombo vya habari (kama vile TV, redio na magazeti) na tovuti ya SECO IFC Leasing Program Tanzania (*www.ifc.org/africa*) ;

(5) Karadha ndogondogo – kushirikiana na taasisi ndogo ndogo za fedha ili kuendeleza karadha ndogondogo ; na

(6) Chama cha karadha Taifa – tumeanzisha chama wa wadau wa karadha hapa Tanzania ambacho kitahusika na usimamizi wa shughuli za karadha kwa nchi nzima, ikiwa ni pamoja na kutetea maslahi yanayohusu karadha.

Manufaa ya Mradi

- Kuweka mfumo wa kisheria ambao utatoa nafuu ya kodi kwenye karadha, taratibu zinazoeleweka za uhasibu kwenye karadha na kuwepo kwa mfumo wa sheria utakaosimamia karadha; ambao haupingani na sheria nyingine zinazohusu karadha;

- Kujenga uwezo wa wakopeshaji wapya kuingia kwenye karadha;

- Kuongeza fursa za karadha kwa makampuni ya ndani na nje ya Tanzania;

- Kuendesha elimu kwa umma kwa kampuni binafsi, taasisi za fedha, taasisi za usimamizi kuhusu karadha, nk; na

- Kuendeleza chama cha wadau wa karadha Tanzania.

SECO – IFC Leasing Program – Tanzania inatumia utaalam wa IFC kwenye karadha, pamoja na miradi mingine na wataalamu wake kuendeleza karadha hapa Tanzania.

UTANGULIZI

1. UMUHIMU WA KARADHA

Karadha huwezesha au husaidia ukuaji wa uchumi kwa sababu karadha huongeza mtaji kwenye sekta ya uzalishaji. Karadha pia huwezesha makampuni binafsi kupata mitaji. Karadha ni njia nzuri ya kuendeleza uchumi unaokua kama wa Tanzania.

Faida za karadha

- Huwezesha kuboresha mitambo ya uzalishaji na kukuza biashara ndogo - wakopeshaji wana nafasi maalum ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wafanya biashara ndogo na za kati ambapo mitaji hiyo huwawezesha wafanya biashara ndogo na za kati kupanua shughuli zao. Karadha hutoa fursa hii kupanua na kupata teknolojia mpya kwa unafuu zaidi;

- Karadha husaidia kuongeza mtaji na mali za kudumu - karadha ni njia mbadala ya kupata mtaji ili kuendeleza biashara. Njia nyingine ni pamoja na mikopo ya benki na masoko ya mitaji;

- Karadha huleta ushindani kwenye masoko ya fedha - karadha haina hatari kama mikopo ya kawaida kwa sababu mali husika huwa kama dhamana. Karadha huongeza wigo wa vyanzo vya mitaji ambavyo vinashindana na mikopo ya mabenki. Karadha ina nafuu ya uandaaji kuliko mikopo ya benki, hivyo huwezesha wakopaji kuongeza mikopo bila kuathiri mitaji; na

- Karadha huongeza mauzo ya mali na mitambo - wateja wapya wanaweza kupatikana kutokana na karadha.

Faida za karadha ni nyingi na bayana kwa nchi ambazo karadha imekuwepo kwa muda mrefu. Hapa Tanzania, sekta ya karadha bado ni changa. Utafiti uliofanywa umebainisha kuwepo kwa karadha kwa kiwango kidogo sana. Matatizo yaliyopo yamebainishwa na yakirekebishwa yanategemewa kusaidia ukuaji wa sekta ya karadha nchini.

Maana ya karadha

1.2 Karadha ni nini?

Karadha ni mkataba wa wadau wawili ambapo mwenye kumiliki mali (mkopeshaji) anampatia mtumiaji (mkopaji) mali hiyo ili aitumie kwa kipindi maalum kilichokubaliwa kwa malipo ya matumizi ya mali hiyo. Kwenye karadha, umiliki na matumizi ya mali hutenganishwa. Karadha humwezesha mkopaji kutumia mali ambayo pengine hana matarajio ya kuinunua kwa sababu ni rahisi kuipata mali hiyo kwa karadha, au kwa kuwa mkopaji hana fedha za kutosha kununua mali hiyo. Kwenye karadha, faida hupatikana kwa matumizi ya mali na sio kutokana na umiliki wake.

Kuna karadha aina mbili, karadha ya fedha na karadha ya uendeshaji. Karadha ya fedha inahusisha wadau watatu ambao ni mkopaji, mkopeshaji na muuzaji wa mali. Mkopeshaji anaweza kuwa taasisi ya fedha kama benki, ambayo hutumika kumwezesha muuzaji na mkopaji kukutana, kisha mauzo hufanyika.

Karadha ya fedha humwezesha mkopaji kutumia mali iliyo kwenye karadha kwa muda mwingi wa matumizi ya mali husika na matengenezo, uchakavu na bima ya mali iliyo kwenye karadha hugharimiwa na mkopaji. Karadha ya fedha mara nyingi haisitishwi kabla ya muda wake, na hivyo inafanana zaidi na mikopo ya mabenki.

Karadha ya fedha



Karadha ya uendeshaji ni karadha ambayo muda wake ni mfupi kuliko muda wa matumizi ya mali iliyo kwenye karadha. Mkopaji hategemei kuinunua mali hiyo na mkopeshaji anarejesha gharama za ununuzi kwa kuiweka kwenye karadha mali hiyo zaidi ya mara moja, na wakati wa kuiuza baada yakutumika kwenye karadha. Gharama za matengenezo, bima na uchakavu ni za mkopeshaji.

Tofauti ya mkopo wa karadha

Kigezo	**Mikopo**	**Karadha ya Fedha**	**Karadha ya Uendeshaji**
Umiliki wa kisheria wa mali	Mkopaji	Mkopeshaji	Mkopeshaji
Kutayarisha matumizi ya mali	Vifaa au mali huwekwa rehani	Umiliki wa mali	Umiliki wa mali

	kwa lengo la kudhamini mali husika au nyinginezo		
Dhima/dhamana	Ni ya juu	Kawaida	Ndogo
Kutunza mali na bima	Mkopaji	Kwa sehemu kubwa ni mkopaji	Mkopeshaji
Hatari (uharibifu, thamani ya mwisho	Mkopaji	Kawaida ni mkopaji	Kawaida ni mkopeshaji
Fursa ya kusitisha karadha	Haipo	Haipo	Kwa kawaida ipo kwenye mkataba

2. Hali ya uchumi wa Tanzania

Tanzania ilianzisha mageuzi makubwa ya uchumi mwaka 1986 yaliyokuwa na lengo la kubadilisha mfumo wa uchumi kutoka uchumi hodhi na kuwa uchumi unaotegemea nguvu za soko. Mabadiliko haya yalisababishwa na matatizo ya mfumo mzima wa uchumi uliokuwepo wakati huo kama vile kukosekana kwa mikopo, usimamizi wa riba, vizuizi kwenye matumizi ya fedha za kigeni, uwekezaji kutoka nje ya nchi na kutokuwepo usimamizi mzuri wa mabenki.

Jitihada za kuongeza ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 5.5 miaka ya 1973-78 hadi asilimia 8.4 miaka ya 1978-82 ilitekelezwa kwa kutumia mpango wa kufufua uchumi chini ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Marekebisho haya yalihusisha kuondoa vizuizi vilivyokuwepo, kuruhusu biashara huria, kuondoa usimamizi wa bei na kuhimiza ushiriki mkubwa zaidi wa sekta binafsi kwenye uchumi wanchi.

Kwa ujumla, jitihada hizi za kufufua uchumi zimeanza kuleta mafanikio. Ukuaji wa uchumi ulifikia asilimia 6.3 mwaka 2004 na 2005. Vigezo vingine kama mfumuko wa bei ulifikia asilimia 5.5 na thamani ya fedha ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani ambayo ilikuwa ni shilingi ya Tanzania. 1,100/= mwaka 2004. Riba za mikopo zilishuka kutoka asilimia 25 hadi 15 ambapo zile za amana zilikuwa 3. Pamoja na mafanikio haya, bado uchumi wa Tanzania uko kwenye hatari ya kutokukua kutokana na utegemezi mkubwa kwenye bei ya mazao yanayouzwa nje, hali ya hewa na kukosekana kwa utawala bora.

2.1. Hali ya huduma za sekta ya Benki nchini

Sekta ya Benki Tanzania imekuwa imara baada ya marekebisho ya mfumo wa mabenki. Kwa sasa kuna jumla ya mabenki 26 na taasisi za fedha tano (5). Mabenki 15 kati ya hayo yanamilikiwa na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Hadi Mei, 2005 mabenki haya yalikuwa na mali zenye thamani ya shilingi za Kitanzania 3.485 bilioni.

Marekebisho ya sekta ya fedha pia yamelenga sekta za bima, pensheni na masoko ya mitaji. Ripoti ya Benki ya Dunia ya Mei 2003 inaeleza kuwa sekta ya fedha ya Tanzania haijachangia vya kutosha kuendeleza sekta hii. Mchango wake haujafikia kiwango kinachotakiwa kuendeleza uchumi wa nchi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za fedha, umiliki wa serikali wa taasisi hizo, marekebisho ya sheria na uwekezaji wa muda mrefu kwenye sekta ya fedha.

2.2. Huduma ndogondogo za fedha

Hali ya mfumo wa huduma ndogo ndogo wa fedha ilirekebishwa kwa kuongeza kifungu chenye kuhusika na taasisi ndogo ndogo za fedha na usimamizi wake kuwa chini ya Benki Kuu. Kanuni za usimamizi wa taasisi hizo zilitayarishwa na kupitishwa na Waziri wa Julai, 2004. Kwa mujibu wa takwimu zilizokuwepo hadi 2003.